**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

# MPANGO WA RAIS MHE. DKT SAMIA SULUHU HASSAN WA KUONGEZA WATAALAMU BINGWA NA BOBEZI WA AFYA NCHINI KWA MWAKA 2024/2025

***"SAMIA HEALTH SPECIALISATION SCHOLARSHIP PROGRAM 2024/25"***

**Dodoma, Oktoba 21, 2024**

**Ndugu Wanahabari;** Serikali ya Awamu ya Sita chini ya **Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan** imeendelea kufanya mageuzi makubwa ndani ya Sekta ya Afya, lengo likiwa ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za matibabu hasa ya kibingwa na ubingwa bobezi hapa nchini.

**Ndugu Wanahabari;** Katika kufanikisha azma ya kuwa na watalaamu wenye ujuzi wa kutosha wa kutoa huduma bora za matibabu hapa nchini, Wizara ya Afya ilijiwekea lengo la miaka mitano (2020-2025) la kusomesha wataalamu bingwa na wabobezi wasiopungua 300 kwa kila mwaka wa fedha kupitia Mpango wa Ufadhili wa Masomo wa Serikali unaojulikana kama '***Samia Health Specialization Scholarship Program***'. Jitihada hizo zimelenga kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya, kupunguza rufaa za matibabu nje ya nchi na hivyo kupunguza gharama kwa Serikali na wananchi pamoja na kuvutia tiba utalii.

**Ndugu Wanahabari;** Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali kupitia Wizara ya Afya imetenga jumla ya **Shilingi Bilioni 14,** ikiwa ni ongezeko la

shilingi **Bilioni 3.05** sawa na **28%** zaidi ya bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ya **Shilingi Bilioni 10.95.**

Fedha hizi zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 zitatumika kugharamia mafunzo kwa wataalamu wapya **544** kwa mafunzo ya Ubingwa na Ubingwa bobezi pamoja na wataalamu wengine **47** kwa utaratibu wa seti. Aidha, wataalamu **829** wanaoendelea na masomo ya ubingwa na ubobezi katika vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi wataendelea kupewa ufadhili kupitia fedha hizo.

**Ndugu wanahabari;** kwa mwaka huu wa fedha 2024/2025, Wizara ilipokea jumla ya maombi ya ufadhili **948** nchi nzima**,** kati ya hao waombaji wa jinsia ya kike ni **353** sawa na **37%** na ya kiume ni **595** sawa na **63%.** Kati ya hao, waombaji **771** walikidhi vigezo vya kufadhili wa na waliochaguliwa kwa ajili ya ufadhili ni **544** sawa na **71%** ya waombaji waliokidhi vigezo.

Kati ya watumishi **544** waliochaguliwa kupata ufadhili, jinsia ya kiume ni **338 (62%)** na jinsia ya kike ni **206 (38%)**. Watumishi waliochaguliwa kupata ufadhili katika vyuo vya ndani ya nchi ni **517 (95%)** na nje ya nchi **27 (5%)**.

Kwa takwimu hizi, kumekuwa na ongezeko la kufadhili watumishi wanaoomba kusomeshwa na Serikali kutoka **56%** mwaka 2022/2023 hadi **71%** mwaka 2024/2025. Serikali ya awamu ya sita kwa kuona umuhimu wa uwekezaji katika Sekta ya Afya imeshatumia jumla ya Shilingi **Bilioni 30.95** katika kuendeleza wataalamu bingwa na bobezi katika sekta ya afya nchini.

**Ndugu Wanahabari;** Wizara imezingatia vipaumbele muhimu vya kisekta kama ubobezi (super-specialization) katika ngazi mbalimbali za huduma pamoja vipaumbele kama vilivyoainishwa kwenye ***Mpango Mkakati wa tano wa Sekta ya Afya (Health Sector Strategic Plan V-HSSP V)*** pamoja na bajeti ya Wizara ya mwaka 2024/25. Taaluma za watoto wachanga (Neonatology), afya ya akili (Mental health), magonjwa yasiyoambukiza (NCDs) kama magonjwa ya moyo (Cardiology), matibabu ya ubongo na mishipa ya fahamu (Neurosurgery), huduma za utengamao na tiba shufaa (rehabilitation and palliative services), ugunduzi wa magonjwa ikiwemo patholojia ni mifano ya vipaumbele vyetu. Hata hivyo kipaumbele kimetolewa kwa watumishi wanaofanya kazi kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa wa wataalamu bingwa kwa kuzingatia uwiano wa kijiografia.

**Ndugu Wanahabari;** Napenda kuwatangazia watumishi wote waliopata ufadhili kwa mwaka 2024/2025 kwamba wanapaswa kukamilisha taratibu

za kujaza mikataba ya ufadhili kama kigezo cha kukubali ufadhili huu kabla ya tarehe **01 Novemba, 2024**. Nakala ya mikataba hiyo inapatikana kwenye tovuti ya Wizara na pia itatumwa kwa barua pepe kwenye anuani walizotumia wakati wa kuwasilisha maombi.

**Ndugu Wanahabari;** Ufadhili huu ni kwa ajili ya kulipiwa ada ya mafunzo na posho ya utafiti kwa watakaofadhiliwa ndani ya nchi. Aidha, kwa wale wanaosoma vyuo vya nje ya nchi watalipiwa ada, posho ya kujikimu wakiwa masomoni (**Stipend**), nauli ya kwenda na kurudi pamoja na posho ya utafiti. Malipo ya posho ya utafiti na posho ya kujikimu yatazingatia viwango vilivyopangwa na Wizara.

**Ndugu Wanahabari;** Nichukue fursa hii kuendelea kumshukuru na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuendelea kuwekeza kwenye Sekta ya Afya hususani katika kuendeleza wataalamu bingwa na bobezi ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata matibabu ya kibingwa na kibobezi yanayotolewa na wataalamu wetu wa ndani. Uwekezaji huu ni wa kimkakati utakaoleta tija kwa miaka mingi ijayo kwa kuongeza wigo wa watalaam bingwa na bingwa bobezi watakaotoa huduma bora kwa wananchi. Hii ni dhamira ya dhati ya Rais wetu **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** ya kuishi Mpango Mkakati wa Tano wa Sekta ya Afya kwa kutomwacha mtu yeyote nyuma **(Leave no one Behind)** katika kuleta maendeleo ya sekta ya afya na nchi kwa ujumla.

Aidha, nichukue fursa hii kuwashukuru wafanyakazi wa Wizara na Sekta ya Afya kwa ujumla kwa kazi kubwa wanayoifanya kuwahudumia wananchi katika ngazi zote za kutolea huduma. Niendelee kuwatia moyo kuwa Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan itaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**

Jenista Joakim Mhagama (Mb)

**WAZIRI WA AFYA**